

**MOMBASA COUNTY ASSEMBLY****HANSARD REPORT**Thursday, 28<sup>th</sup> July, 2016

The House met at 2.38pm-3.54pm.

*(Hon. Deputy Speaker (Mr. Mswabah Rashid) in the Chair)***PRAYERS****Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Members you may seat down.Clerk?**STATEMENT**

Hon. Zainab S. Githinji, not there, Leader of Minority?

**Leader of Minority Hon. (Ms.) Maimuna Salim:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama ku wakilisha taarifa ambayo ilikuwa imeletwa na Mheshimiwa Zainab sababu hasikii vizuri amepelekwa hospitalini.

Mheshimiwa Spika taarifa ni kuhusu sisi kama serikali ya Kauanti ya Mombasa tuko na mamlaka ya kuweza kuweka mambo ya...(??), sisi tuko na mamlaka ya kuangalia usalama kwanza.

Pili sisi kama serikali ya Kaunti ya Mombasa tunaona vile vitu vya kuangalia usalama ambavyo ni CCTV havitufanyii kazi kulingana na vile tunavyo fikiria kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanatendeka na watu wakiitisha zile stakabadhi za CCTV kuangalia si rahisi kupata hiyo ripoti ya CCTV.

Kwa hivyo sisi kama serikali ya Kaunti ya Mombasa inatakikaniwa ya kwamba tuweze kuwakilisha kuweka katika maeneo tunayoishi vichochozoni kwa sababu kama sehemu hizo za Kisauni kuna wale vijana ambao wanajiita wakali kwanza.

Vijana wale ambao ni wahalifu Kaunti ya Mombasa lakini tukitaka kuwafuatilia kwa zaidi hatuwezi kuwapata unasikia tu vijana wamefanya kitendo hapo na watu wamemwangalia na ameondoka.

Kwa hivyo sisi tulikuwa tunaomba ya kwamba kuweza kuwekwa CCTV katika mitaa katika Kaunti ya Mombasa yote ili jambo lolote la uhalifu kama juzi hawa vijana walivyoweza kuuliwa Mheshimiwa Spika ingekuwa ni CCTV yetu ingekuwa imeweza kutupatia kama ni magari mangapi na walienda kivipi na walipatikana kivipi.

Kwa sababu watu wengine pia wanakufa kiholela holela kwa sababu zile CCTV zina kuwa *controlled* na serikali kuu ama zina kuwa *controlled* na *national security*; sisi kama Serikali ya Kaunti tunatakiwa tuziweke na ziwe zina kuwa *controlled* na serikali ya Kaunti ya Mombasa kusudi ili yule mtu mnyonge zaidi aweze kuwakilishwa na hao vijana ndio tutaweza

kuwakomesha na pia sisi itakuwa ndio njia moja ya kuweza kuangalia hali ya usalama. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Fadhili Makarani what is it?

**Hon Mwalimu:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika ndani ya hoja zetu tano inaturuhusu leo tutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika mimi ningependa Kiongozi wa Walio Wengi aelezee Jumba hili ni hatua gani serikali ya Kaunti ya Mombasa imechukuwa kutokana na visa ambavyo twaviona vinaendelea.

Katika mashule Mheshimiwa Spika tumeona mashule katika Kaunti zingine zikichomwa nataka tujue Kiongozi wa Walio Wengi Mheshimiwa Spika aeleze Jumba hili serikali yetu inachukua hatua gani kufikia sasa hivi Mheshimiwa Spika...

*(Interruption)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Ndanda Chiro?

**Hon. Mohamed Ndanda:** Mheshimiwa Spika ningependa anayezungumza Mheshimiwa Fadhili Makarani atueleze kama Mombasa kuna shule yoyote iliyo chomeka kwa sababu Kiongozi anayeongoza Walio Wengi katika Bunge hili anaongoza Kaunti ya Mombasa sasa kama yeye labda ni wa Kenya nzima.

Pia atuambie maanake mimi hivi hivi punde sijasikia wanafunzi wetu wana nidhamu sana Mheshimiwa Spika, sijasikia wamechoma.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Mary Akinyi.

**Hon. (Ms.) Akinyi:** Ahsante Mheshimiwa Spika, mimi ningependa Mheshimiwa Fadhili ambaye alikuwa aendelee kutoa taarifa aendelee kutoa kwa sababu hayo mambo ya shule kuchomwa ni janga la Kenya nzima si ati ni ya Kaunti ya Mombasa peke yake, kwa hiyo ningependa aendelee.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Before Hon. Fadhili continues with what he was talking, we have a statement by Hon. Zainab S. Githinji which was brought here in the House by the Minority Leader.

I have to make a judgment on that we have to find a solution on how to commit that matter to the Committee which is concerned with that business.

So ladies and gentlemen the statement on insecurity in County on CCTV to the Committee concerned with security; we need to know whether these CCTVs, whether the County government can put our own CCTVs and so the Chairman of the Committee of

---

**DISCLAIMER:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 2*

---

Administration should take over the issue within two weeks you take up the matter Hon. Ndanda Chiro.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Saad Faraj.

**Hon Faraj:** Mr. Speaker thank you. Mr. Speaker there was a similar matter that was brought here last week and the Committee in charge of Security was given that opportunity to be able to go to the ground to verify the situation and the status so that we can get back the report.

Mr. Speaker I think that this issue which has been brought up as a statement by the Minority Leader on behalf of madam Githinji is a similar kind of a statement which needs to be addressed.

I agree that it needs to be addressed but Mr. Speaker we cannot give more time to the Committee because of the fact that this issue and the issue that which was raised last week are similar.

Mr. Speaker I think may be with your guidance if we are to give them any time or rather the timelines that are needed for this issue to be down should be within at least a period of about two weeks including the job which was allocated to them last week Mr. Speaker, thank you.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Patrick Siminyu.

**Hon. Siminyu:** Mr. Speaker this House had been talking about security all the time and the Committee that is headed by Hon. Ndanda from Kazandani has already started the process and it has already started talking to the community in charge in the matters apartaining to *wakali kwanza* and they have already gone for the site visit.

Mr. Speaker I think this thing has to be dealt with as a whole because the issue of CCTV is the police that are in charge, we have the issue of Inspectorate and if it comes to things like these we know it will be a pity on them.

Mr. Speaker, I think the Committee should be given a mandate to look into the issue because just yesterday we had an issue of cars being vandalized and it is the same issue to do with security and it was given to another Committee, another Committee was formed, we need to have a clear direction so that we can have a comprehensive report which is going to touch on the matter of security, so that we can have solution to the people, thank you Mr. Speaker.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Ndanda Chiro.

**Hon. Mohamed Ndanda:** Thank you Mr. Speaker, on matters of clarity Hon. Speaker, as a matter partaining to the previous work it was very special for some areas, but for this one now

which is raised by Hon. Maimuna, the Minority Leader it talks on the CCTV which is all over Mombasa County.

But the previous order I was told to go and investigate and acquire information on matters of sexual harassment to ladies which we are in the process and today we managed also to visit the area and comprehensive report will be brought to this parliament at this Assembly next week as agreed in the House Business.

Otherwise I don't feel that it will be too much work and waste of funds because we have to follow item by item and make sure this report to this House is fully informed so with me as the Chair I don't doubt the statement Hon. Speaker, only through your guidance because I see Members are now becoming Speakers in this House and also they want to mislead the whole system of this parliament.

So Hon. Speaker it is your turn now to take up your Chair and guide us accordingly, otherwise let us see the difference between the CCTV in all over Mombasa County, the government and the one which was raised by Hon. Fatuma Kushe which is from Kisauni and it is being worked on, that is in the kitchen being prepared thank you very much.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Tom Ogalo.

**Hon. Ogalo:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ningeomba Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama aende pia Timbwani kwa sababu *wakali kwanza* wako pia Timbwani, aende pia achunguze kwa sababu vile wanafanya huku Kisauni ndio wanafanya Timbwani, asiende mjini peke yake, aende pale Timbwani pia ningeomba.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Okay Hon. Ndanda I think the issue of security is very important. Yes Hon. Sarah Nyamvula what is it?

**Hon. (Mrs.) Nyamvula:** Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker whether women are being harassed or its *wakali kwanza* the use of CCTV is important.

Mr. Speaker my opinion is this is an issue with the security of the County of Mombasa, the way it happens the type of harassment or the type of abuse is different to fall under security.

So I want the Chairman of Security; by the way congratulations, come out and say specifics now you can see the Hon. Member representing Timbwani saying it's in Timbwani.

For me Frère town I will say it's in Shelemba, its in Barisheba so this CCTV is there to assist us in recognizing and identifying the issue of insecurity, kindly and this is not as the Chairman says, Chairman of Security we are trying to be the Speaker no, we are not trying to be

the Speaker here, we are both representatives of the people and we see we can only debate and contribute in what we see, what we see is insecurity all over we are going to say so.

I think we specifically through what Hon. Fatuma Kushe brought last week we actually..., and I remember my contribution I even told..., I did say to this House that the issue is the young men are very unfortunate and these are our children and grand children and it is us parents who move them when things happen.

So you see the movement of this insecurity within Mombasa and let me say this, it is actually coming to the Island because if I live here my kid is picked up or my grandchild is picked up, my initial way of doing things is to sympathize with that child, if that child has got a relative in Kilifi, Kwale we send them there.

Mr. Speaker this is insecurity wholesomely. Thank you Mr. Speaker.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Jimmy Odari.

**Hon. Odari:** Thank you Hon. Speaker. Hon. Speaker the issue of security is quite a critical matter that should be taken with the seriousness that it deserves.

I'm happy that the Hon. Speaker, the Hon. Member who has spoken has mentioned about Kilifi County because she is a resident in Kilifi County and there is nothing bad about it because insecurity as she rightly pointed out is everywhere.

Hon. Speaker insecurity in Mombasa is in such a state that this County needs to take very pragmatic steps.

I want to thank the government in collaboration with safaricom for the CCTV cameras which have been placed in some areas of this County but I think it is not enough, if we have those cameras everywhere including the areas which are critical which are known to be hotspots for insecurity.

Hon. Speaker, even this Assembly; this Hon. House is very insecure, people are entering this Assembly like they are entering the toilet, because there is no check up even right now at the gate there.

If in a supermarket people are screened before entering any supermarket or any office in town you are screened, here nobody is being screened, every Tom, Dick and Harry enters here, here there is no CCTV around here and even am very scared for this Hon. House in which Members who are representing 1.3 million residents of Mombasa are seating can be attacked anytime, it is very serious, we need to take this matter very seriously to be done with the urgency it deserves.

We need to take very drastic actions so that the Assembly is secured, and even the entire Mombasa County is all secure.

This will create a conducive place for the people of Mombasa and also an internationally known tourist destination so that it may enhance that image, so that to attract more tourists to this County, thank you Hon. Speaker.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Siminyu.

**Hon. Siminyu:** Mr. Speaker, the issue of CCTV is a solution to the Hon. that we are discussing.

Mr. Speaker just what i would say, that's why am saying in the report that we are looking for a solution on how we can tackle the insecurity problem that we are facing.

Mr. Speaker the report might come with a solution; the systems that should be placed so a repeat of this... so this Committee does have a chance to talk with the Security Officer to let us know the police procedure or the institution concerned with security matters.

It is important if this Committee is sent outside there to go and bring a comprehensive report; if it is the shortage of the CCTV cameras then we want to know or if there's a problem of sharing information of the CCTV.

And if the County Government while you are sitting in the Inspectorate department is it possible to install our own CCTV so that we can manage Mr. Speaker? This can be done accordingly. Thank you.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Omar Ebrahim (Meti).

**Chief Whip** (Hon. Ahmed Ebrahim Omar): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Spika kabla ya maendeleo kufika mahali popote lazima kuwe na usalama; sisi kama Mombasa unajua Kaunti yetu ni Kaunti inayotegemea sana utalii sababu tuko na mahoteli mengi na tuko na historia kubwa sana.

Lakini jambo la ukosefu wa usalama Mheshimiwa Spika hilo jambo limefanya shughuli zetu za mahotelini kupungua na hivyo zafanya ajira zipungue katika Kaunti yetu.

Mheshimiwa Spika hivi juzi siku ya Ijumaa kuna kijana wangu mmoja alikuwa anatoka masomo ya ziada yaani *tuition* usiku kama kipindi cha saa nne akavamiwa na majambazi akadungwa kisu kwa tumbo, viwili mgongoni, lakini twashukuru kijana mwenyewe hakupoteza maisha hata niliweza kumsaidia kulipa fedha anazodaiwa Hospitali ya Mkoa ya Coast general.

Kwa sababu ni kijana wa kidato cha tatu na wakati alipokuwa spitali alikosa masomo Mheshimiwa Spika kwa sababu kijana yuko pale spitali na wenzake wanaenda shule.

Ni kama hujuma Mheshimiwa Spika ni lazima sisi kama viongozi wa Mombasa tuongeze bidii yetu tuangalie mambo ya usalama.

Hili jambo la CCTV ni jambo muhimu sana; mwanzo kama tunasikia kuna *wakali kwanza*, *wakali wao* na wengine pia hata majina siyajui yaani kuna makundi mengi ya vijana ambao wanakaa maskani wakitumia stimu na wanaanza kuleta maafa kwa jamii yetu Mheshimiwa Spika.

Kwa hiyo haya mambo ya CCTV Mheshimiwa Spika lazima tuyatilie maanani sana hata katika Jumba letu la Mombasa tuangalie maduka ya *supermarket* ukiingia lazima uangaliwe hata kuna zile kama kwenda kwa hoteli kama mashine ya *dictate* vile ukiingia lazima iangalie kama kuna kitu chochote kibaya lazima uweze kukaguliwa ndio uweze kuingia katika sehemu kama ile.

Mheshimiwa Spika sisi tumezungukwa na maadui wengi sana nafikiri kama hatujui basi ni lazima tukumbushane sio watu wote wanaotutakia mazuri na mambo ya ugaidi ni mengi sana.

Mheshimiwa Spika leo hii hata kukiingia hata gaidi awe amejifunga bomu lake sisi sote twende mpaka wewe uliyekaa kwa hicho kiti kwa sababu lazima jambo hili tuliangalie kwa makini ya kwamba usalama ni lazima tuanzishe kwa hii Nyumba kuwekwe CCTV kwa zile sehemu zinazohitaji ili tuweze kumaliza jambo la ukosefu wa usalama katika Kaunti ya Mombasa ili tupate maendeleo, tupate watalii kama vile kitambo walikuwa wakija kwa wingi Mheshimiwa Spika.

Vile vile watalii wakija ndio ajira za vijana zitapatikana na pia ukosefu wa usalama utaweza kupatikana. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Paul Onje.

**Hon. Onje:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika jambo la CCTV ni jambo la maana sana na inafaa sisi kama Waheshimiwa wa Kaunti ya Mombasa tuzingatie.

Kwanza nikianza na na mahali tulipo Mheshimiwa Spika maanake tunaongea juu ya usalama wa Kaunti ya Mombasa hatuwezi kuongea kuhusu usalama wa Kaunti na hapa mahali tupo ambapo tunaangalia maslahi ya wananchi na sisi ni Wawakilishi na hatuwezi tukaangalia kwanza hapa pekee yake ndio tuko na shida kwanza manake hii Assemblies yetu yote ukiingia hata kwenye *corridor* kila mahali hatuna CCTV yeyote ambayo inaweza kutuonyesha kitu gani kinaendelea, ama ni nani anaingia hata mtu akifanya jambo fulani.

Juzi juzi kuna tarakilishi ziliibwa hapo kitengo cha *Accounts* hatuwezi kujua ni akina nani waliiba hizo? Juzi juzi *Mace* iliibiwa ikaenda kufichwa huko....

*(Laughter)*

Kama kungekuwa na CCTV...

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika tungejua ni nani amechukua? na tungeenda kwake na tumwambie atupe *Mace* yetu na tuendeleo na Assembli yetu.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika tunaongea mambo mengi sana lakini tunasahau yale ambayo yatatusaidia sisi kama waheshimiwa wa Kaunti ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika nikitaka kukumbusha wakati tulikuwa kule kwenye ofisi ya Kiongozi wa Walio Wengi unajua kulikuja waizi ambao walikuja pale na waliletwa na watu ambao siwezi kusema kwa saa hizi.

Tulipokuwa tunataka kumtoa aliyekuwa Kiongozi wa Walio Wengi Bungeni na kutaka kumueka Kiongozi wa Walio Wengi mpya ambaye tuko naye saa hii kuna wahuni ambao waliweza kuingia pae Mheshimiwa Spika na wengine wao walikuwa na visu.....

*(Laughter)*

Walitambulika na kuna wengine niliona kidogo hata kama walikuwa na mbao lakini ilikuwa ni kama bastola hakuna CCTV lakini mimi niliona.....

*(Laughter)*

Kwa hivyo tukiona mahali ambapo tuko hapa itakuwa ni vyema zaidi ndio tukitoka nje ama tukipeleka usalama nje Mheshimiwa Spika tutajua vile tutakavyofanya.

Leo hii mtu akipatikana na shida hatutajua vile tutakavyofuatilia na itakuwa ni aibu sana manake yale ambayo tutakuwa tunaangalia ni mambo madogo madogo sana lakini usalama wetu tumeshindwa kuuweka mbele Mheshimiwa Spika mpaka hata kule nje waheshimiwa wanalia magari yanaibwa, wanaiba zile *side mirrors*, zile *logo* wanaiba na wanaenda nazo huko lakini hapa ndio inasemekana kwamba sisi ndio watungaji wa sheria na sisi ndio tunawakilisha watu wa Mombasa na ilhali sisi wenyewe tumeshindwa kujiwakilisha.

Mheshimiwa Spika inakuwa ni aibu lakini nikirudi kwa mambo ya kusambaza CCTV kule mashinani hiyo ni haki yetu kama Wawakilishi wa hii Kaunti Assembli; hiyo ni haki yetu kabisa manake serikali ni serikali, ni serikali kabisa ikiwa serikali kuu wameweka yao sisi pia tutaongeza yetu....



(Applause)

Inawezekana serikali kuu wanaweza angalia kupitia kwa CCTV yao wakati sisi tukiomba watatuambia kuwa kulikuwa na giza giza mambo inapotea hapo hapo lakini tukiwa na yetu tutawaambia kama yenu ilikuwa na unyevu unyevu lakini yetu iko wazi na huyu ndio alikuwa anafanya maneno na hapo itakuwa tumesaidika.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika tutangalia, mimi naona tunaweza kuangalia ni Kamati gani inaweza kuangalia hilo swala na wakae chini waangalie Kaunti ya Mombasa nzima kabla tufike kwa hii Nyumba tunaomba Mungu *InshaAllah* mambo kama yatakua sawa hiyo pesa ikija wale watakaokuja waweke kwa mambo ya dharura mambo yaende mbele, ahsante.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Hatimy.

**Hon. Mohamed Hatimy:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kidogo naona kuna shida, ni sisi serikali yetu ya Kaunti ya Mombasa, katiba chini ya kifungu *Article 6, (2), 'The government's at the national and County levels are distinct and inter-dependent and shall conduct their mutual relations on the basis of consultations and cooperation'*.

Mheshimiwa Spika tulianza vizuri sana kuwa Mombasa ilikua Kaunti ya kipekee; Kaunti ya kwanza kuingia mkataba wa makubaliano na Gavana wetu alijaribu kuleta magari alioleta na vifaa vingine nafikiri itakua jambo la busara hivi sasa tuko na Kamishna mpya ambae tuko nae ikiwa Kamati ya Mheshimiwa Mohamed Ndanda ataweza kufanya kuchukua majukumu kwenda kukaa na huyu Kamishna kuzungumzia juu ya Kaunti kuambia serikali usalama inavyoenda.

Kwa sababu Mheshimiwa Spika kuna mambo mengine...ule ukweli lazima usemwe chini ya kifungu *Article 185, 186 na 187* ya Katiba iko wazi ambayo majukumu ukiangalia kwenye *Court schedules part one paragraph seven* ya Katiba iko wazi kuwa hili ni jukumu la serikali kuu.

Kwa hivyo mimi naomba Nyumba hii tukubaliane ya kuwa Mheshimiwa Ndanda na Kamati yake waweze kwenda kuonana na Kamishna tulienae sasa Bwana Maalim waangalie kwa sababu kuweka CCTV kwa hivi sasa Kaunti sisi hatuna uwezo, ni pesa nyingi sasa hatuna uwezo...

(Interruption)

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Paul Onje.

**Hon. Onje:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika yangu nasimama na *point of information*, Mheshimiwa mwenzangu anaongea vizuri lakini kuna mahali amesahau ndio nataka niweze kufafanua kidogo, usalama wetu wa Bunge la Kaunti haifai sisi kwenda kujulisha serikali kuu...

(Laughter)

Yetu ya Bunge la Kaunti ni yetu hapa kwa hivyo tukitaka kuweka CCTV hapa sio lazima tuende serikali kuu, hiyo ni mambo yetu sisi hapa...

*(Laughter)*

**Hon. Mohamed Hatimy:** Nafikiri Mheshimiwa Spika hii ilikua *point of mis information*.....

*(Laughter)*

Kwa sababu Katiba imetuambia kuwa wakati wowote hata ikiwa jukumu ni la serikali luu unaweza kwenda kuomba ukapewa na sisi hatuja uwezo kusema kuwa twaweza kutoa usalama ndani ya Kaunti yetu.

Kwa hivyo ni lazima sisi tushirikiane na serikali kuu ili tupate matakwa yetu tunayoyataka ndipo hapo Gavana akienda kutia sahihi ya makubaliano na Waziri wa Usalama kuwa tutafanya kazi pamoja tuhakikishe kuwa Kaunti yetu iko na salama kwa sababu bila usalama hakuna mtu yoyote atakayekuja kwenye Kaunti yetu.

Mheshimiwa Spika kwa hivyo jambo la kwanza ni usalama ndani ya maisha ya Kaunti yetu, kwa hivyo mimi naomba Kamati ya usalama iweze kuonana na Kamishna kukaa na kuweza kuzungumza kuangalia vipi tutaweza kushirikiana na kuweza kupena usalama kwa wananchi wetu wa Mombasa.

Mheshimiwa Spika pia nataka kusema kuwa jambo hili sio pahala pamoja twataka ile taarifa iliokuja na Mheshimiwa Maimuna naomba irekebishwe kuwa jambo hili lina athiri Kaunti ya Mombasa na sio pahala pamoja, kwa sababu juzi katika magazeti kuna kila *Sub County* imetajwa vile vikundi vilivyoko.

Kwa hivyo imezungumzwa kwa Kaunti nzima wala sio Kisauni peke yake wala Likoni peke yake lakini ni Kaunti nzima inahitaji mambo ya usalama yatiliwe nguvu ili tuwe na amani kwa Kaunti yetu, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Amir Thoya.

**Hon. Thoya:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa ajili ya kuunga mkono hoja ambayo iko katika Nyumba yetu tukufu.

Masuala ya usalama ni masuala ambayo ni nyeti sana pamoja na kwamba mwaka wa 2015 kwa mara ya kwanza katika historia kuweza kuleta historia tuliweza kuleta mswada wa kufunguliwa kwa kitengo maalumu cha masuala ya polisi katika Kaunti yetu ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika mswada huu uliweza kuletwa Bungeni na uliweza kupata upinzani mkubwa kutoka kwa serikali ya kitaifa kwa sababu wao walisema ya kwamba masuala ya

---

usalama yako katika ngazi za serikali kuu lakini Kaunti yetu ya Mombasa ina changamoto ya kiusalama ambazo hazionekani katika Kaunti zengine zozote katika taifa letu tukufu la Kenya.

Mheshimiwa Spika ni katika Kaunti ya Mombasa peke yake unaweza kuona kijana anapigwa risasi hadharani kwa sababu ya tuhuma za ugaidi, ni katika Mombasa peke yake ambapo kundi za vijana kama *wakali kwanza*, *wakali wao* wananyonya matiti hadharani ya mama zetu.

Ni katika Kaunti ya Mombasa peke yake ambayo ina kitengo cha Polisi ya kuangalia masuala ya utalii, ni katika Mombasa peke yake kuna vitengo mbalimbali ambapo haviko katika Kaunti nyengine.

Kutokamana na hili Mheshimiwa Spika ni dalili ya wazi kwamba Kaunti ya Mombasa masuala ya usalama yako tofauti na Kaunti zengine.

Kwa hivyo ikiwa twasema katika Kaunti yetu kwamba iko haja ya dharura kwamba usalama wa kwetu uwe tofauti na za Kaunti zengine.

Kwa hivyo tunaposema kwamba ni muhimu kwamba Kaunti yetu ya Mombasa iweze kuweka vitengo vile ambavyo vya CCTV ili uhalifu wowote unafanyika tuweze kuhakikisha kwamba tunauona sisi wenyewe; serikali ya Kaunti iweze kuweka CCTV lakini ni masikitiko kwamba kama serikali hatuwezi kuwa na njia ya kuangalia ni aina gani ya uhalifu inaonyeshwa katika vile vyombo vya CCTV ambayo ina shikiliwa na serikali kuu.

Kwa hivyo ni muhimu kama Kaunti yetu ya Mombasa inaweka askari wa trafiki, yafanya kazi vizuri ya serikali ya kitaifa ni muhimu tuweze kuwa na vitengo vyengine vilevile vya usalama ambavyo vitafanya kazi ambavyo vitafanya kazi na serikali ya kitaifa ili tuweze kuwa na usalama katika Kaunti yetu.

Kwa hivyo cha msingi ni kuweza kuunga mkono swala kama hii ambalo limepitishwa na Bunge letu ili tuhakikishe tuweze kutenga fedha maalumu ili tuweze kuhakikisha vitengo kama hivi vinafanya kazi katika Kaunti yetu ya Mombasa, Kaunti yetu iko tofauti lazima tuhakikishe kwamba imekua tofauti katika mikakati ya usalama, ahsante Bwana Spika naunga mkono mia fil mia.

*(Applause)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Leader of Majority. Hon. Ogalo you have talked a lot.

**Leader of Majority** (Hon. Mwidani): Ahsante Bwana Spika, mimi naunga mkono.

*(Interruption)*

**Hon. Mohamed Hatimy:** *(Inaudible)*.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Leader of Majority?

**Leader of Majority** (Hon. Mwidani): Ahsante sana Bwana Spika, mimi pia naunga mkono hii taarifa ambayo inaendelea kwa sababu mimi pia naunga mkono hii taarifa inayoendelea kwa sababu...

*(Interruption)*

**Hon. Mohamed Ndanda:** Point of information Mr. Speaker?

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Ndanda Chiro.

**Hon. Mohamed Ndanda:** I think the statement has not been proposed to be discussed by the Speaker; I think the intervention is that you want matters to be clarified, from there Members went on to discuss.

In fact it was Hon. Fadhili who was up with his statement, I do not know whether it is procedural for this House now going on discussing and contributing, even the Majority Leader is now supporting without a proposed statement before...

*(Interruption)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Nyamvula?

**Hon. (Mrs.) Nyamvula:** Mr. Speaker I am actually very surprised the Honorable on the floor just a few minutes ago indicated...and we are trying to be speakers sorry now he is doing the same...

*(Interruption)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. Fadhili what is it?

**Hon. Mwalimu:** Iko haja ya kuangalia wale wote ambao wako in *acting position*...

*(Interruption)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Fadhili we are yet to finish this, Mheshimiwa Spika pole Mheshimiwa Fadhili...

*(Laughter)*

Sorry I am used to the other side, yes Hon. Fadhili we are yet to conclude this topic so you will hold your horses so Members under Standing Order number one I can allow this statement.

It is very important and that is why I have allowed, under Standing order number one for it to be discussed because it is very important.

In the same context Hon. Tom Ogallo I give you one minute because someone came but you are late, i just give you one minute to add to what you have said.

**Hon. Ogallo:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika nilikuwa nataka kuongeza kitu kidogo; mimi siamini serikali kuu ,kwa sababu kila kitu ni siasa unapata wezi kwa *Mpesa* na polisi wako pale Likoni wanaiba pale na pale na polisi wako.

Mheshimiwa Spika mimi siamini naona kuna siasa hii si sehemu inayoshangilia siasa ya Jubilee sasa wanataka kuleta fujo kidogo.

**Hon. Deputy Speaker (Mr. Mswabah Rashid):** Thank you very much Hon. Members; this matter of security is very important, as I said earlier and we have about three statements concerning the same.

I think this one on Committee on Security and this one on expanding the coverage of CCTV is a very important statement so I think Hon. Ndanda Chiro you should try to combine even though the second one you do not need to travel much because you only need to encounter, I think it's the County Secretary or any Minister concerned with security.

But I think it is the County Secretary just go and see the County Secretary to reach out to donors to see how we can expand the CCTV coverage in the suburban areas of this County because they are connected to the urban areas of this County.

So we want them committed to the suburban areas as well; am also of the opinion that *wakali kwanza, wakali wao, wakali* so forth are not only restricted in Kisauni area but are also in Timbwani as the MCA for Timbwani has said and also another area I think Hon. Zainab Said has said so.

I think you should expand the coverage and bring a report in this House so I think two weeks is enough, I know you are a very hard working person and you will work with speed and I think two weeks is enough to bring all the reports together.

Thank you. Members I acknowledge we have a nominated MCA Hon. Aslam Khan from Kisumu...

*(Hon. Khan bows)*

*(Applause)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): We acknowledge your presence here and you are our guest here and we all say welcome to Mombasa County Assembly and this is how we conduct business. Yes Hon. Fadhili what is it?

**Hon. Mwalimu:** Mheshimiwa Spika wakaazi wa Shelemba, wakaazi wa Timbwani watashukuru na uamuzi wako lakini sijui kazi itafanyika vipi kwa sababu ya giza...

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Walio Wengi aweze kutueleza...

*(Interruption)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Yes Hon. of Timbwani?

**Hon. Ogalu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika ningependa Mheshimiwa Fadhili aseme ni mahali gani kuna giza labda Port Rietz kule lakini pande hii yote ya Timbwani inawaka.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Fadhili.

**Hon. Mwalimu:** Ahsante Mheshimiwa Spika tumeona mashule yakichomwa, tumeona zinasongea na zinafika Kaunti jirani.

Mimi nimesimama na ningetaka Nyumba hii iweze kuelezewa na Kiongozi wa Walio Wengi, jee serikali imepanga mikakati gani kuangazia janga kama hili Mheshimiwa Spika, tukielewa kuwa pia sisi tuko na watoto kwa mashule kama yale wengine wanasoma shule kama zile shule zao zimefungwa wako nyumbani.

Ndani ya Kaunti yetu kuna shule za mabweni, ndani ya Kaunti yetu kuna mashule pia ni shule kama zingine kabla ya janga lile halijaingia ndani ya Kaunti yetu tunataka tujue kupitia kwa Kiongozi wa Walio Wengi aweze kutuelezea ni mikakati gani ambayo imeweza kuwekwa na wizara ya elimu kupitia kwa idara ili kuweza kuhimidi janga kama litakapo kuingia ndani ya Bunge letu. Ahsante.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Hon. Leader of Majority do you have an answer to that? I think I will give you a week because it is a very sensitive issue as well, do you have an answer to that?

**Leader of Majority** (Hon. Mwidani): Mr. Speaker how can I have an answer while nothing has happened in the County or any school within the County.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Maybe pre emptive measures?

**Leader of Majority** (Hon. Mwidani): If its pre emptive measures then give me time but actually I know in Mombasa County there is no school that has been burnt.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Then I am giving you a week, not a week but on Thursday with the information whether the County government in collaboration with the national government whether they have any pre-emptive measures.

*(Hon. Mwindani bowed)*

Members I think I would like to rest that issue, Hon. Amir Thoya what is it?

**Hon. Thoya:....**Security Hon. Speaker.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): That one has been overtaken by events, Hon. Fatuma Mote?

**Hon. (Ms.) Fatuma Swaleh Mote:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kunipa fursa hii. Mheshimiwa Spika mimi pia nina taarifa ningependa nizungumzie kulingana na umasikini ulioingia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika ningependa kuzungumzia shule za watu binafsi ambazo zinawafukuza watoto mara kwa mara.

Lakini pia watoto hawa wakifukuzwa shuleni hawaambiwi ...wiki mbili kwa hivyo hiyo wiki mbili hautalipia ambayo umekaa nyumbani utalipia hizo ambazo utakuwa katika shule ni jambo la kusikitisha sana ningepomba idara ya elimu....

*(Interruption)*

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Hon. Fadhili stop being cheeky please.

**Hon. Fatuma Swaleh Mote:** Ningeomba watu wenye hizi shule za binafsi waweze kufikiria wazazi manake kuna wazazi wengine mpaka wakaange viazi, wengine wanauza samaki lakini kwa ufupi wazazi wanataka kusomesha lakini hawana ule uwezo.

Lakini shule wanalipa kiwango cha pesa kidogo kidogo waweze kukubaliwa kulipa pesa za shule kidogo kidogo na watoto wasiweze kufukuzwa shuleni. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Thank you very much, on that matter Chairman Committee on Education you take up the matter and bring it in two weeks time. Yes Hon. Mary Akinyi what is your statement.

**Hon. (Ms.) Akinyi:** Ahsante Mheshimiwa Spika, taarifa yangu ni juu ya kuchelewa kwa kutolewa kwa vitambulisho.

Nimepata malalamiko mengi kuwa siku hizi hata kitambulisho cha mtu kikiwa kimepotea akienda kutafuta anaagiziwa rudi baada ya mwezi mmoja, rudi baada ya miezi miwili anamaliza hata miezi sita kabla hajapata vitambulisho na tunajua kwamba mwananchi yeyote wa Kenya

anatakiwa kuwa na kitambulisho na pia kwa vile tunaelekea mwaka wa uchaguzi watu watataka kujisajili kama wapigaji kura na vitambulisho vinacheleweshwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika nimepata malalamishi mengi sana kwa hivyo ningepomba mwakilishi wa vitambulisho atusaidie katika hilo wazo aweze kutusaidia ni sababu gani vitambulisho vinachelewa kutolewa watu wanaenda wakirudi; wanaenda Huduma wanarudi wanakosa vitambulisho wanaenda kule kwa Sub County wanako sajili vitambulisho pia wanakosa na wamesajili na kila wanapoenda wanaambiwa vitambulisho havijapatikana.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ningepomba hilo jambo tulichukulie maanani na tuweze kulishughulikia tuweze kusaidia wale wenzetu kule nje ambao hawapati vitambulisho mara kwa mara.

**Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Thank you very much Hon. Mary Akinyi I think that is an important issue and Hon. Leader of Majority should take the matter and report to this House in two weeks.

*(Applause)*

**Leader of Majority** (Hon. Mwidani): Most obliged.

**Hon. Deputy Speaker** (Mr. Mswabah Rashid): Clerk?

#### **ADJOURNMENT**

The House rose at 3.54pm.